

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS –TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**

HALMASHAURI YA WILAYA YA MTAMA

(Barua zote zitumwe kwa Mkurugenzi Mtendaji Wilaya)



Simu. Na. 220 2325/2261
Fax Na. 220 2472
E-mail: ded@lindidc.go.tz



Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji (W),
306 Barabara ya Masasi,
S. L. P. 328,
65183 MTAMA-LINDI.

Unapojibu tafadhali taja:

KUMB. Na. LGA/052/2022/2023/NCS/01

07/09/2022

**TANGAZO LA ZABUNI YA UENDESHAJI
WA GHALA LA MTAMA KWA MSIMU WA
MWAKA 2022/2023**

Kampuni ya Mtama DC Investment Company Limited ya Mtama Lindi inakaribisha maombi ya wazabuni shindani kwa wazabuni waaminifu na wenye uwezo wa kazi za msimu wa Korosho kwa mwaka 2022 kama ifuatavyo:-

- i. Mwombaji awe na Leseni ya kuendesha ghala kutoka Bodi ya Usimamizi wa Stakabadhi za Ghala Tanzania
- ii. Mwombaji awe na uzoefu wa utendaji kazi katika mfumo wa stakabadhi za ghala katika mazao ya korosho na Ufuta na Kampuni iwe haijatengeneza hasara kwa miaka miwili mfululizo na pia awe na uwezo wa kujiendesha.
- iii. Mwombaji aambatanishe nakala ya cheti cha uthibitisho wa mmiliki mwenye nguvu ya Kisheria (POWER OF ATTONEY)
- iv. Mwombaji awe na nakala ya cheti cha ulipaji kodi nchini (Tax clearance)
- v. Mwombaji aambatishe taarifa za kibenki za miezi sita kuanzia Machi, 2022 hadi Agosti, 2022.


vi. Muombaji anatakiwa aonyeshe atalipa kiasi gani kwa kila kilo moja. Hata hivyo hatulazimiki kuchukua mzabuni aliyeoomba kwa fedha nyingi.

vii. Maombi yatumwe kwa anuani ifuatayo:-

Katibu wa Bodi ya Zabuni,
Halmashauri ya Wilaya ya Mtama,
S. L. P. 328,
LINDI.

viii. Ada ya zabuni ni shilingi laki mbili tu (Tshs 200,000/=) ambayo haitarudishwa hata kama ombi lako halitakubaliwa, ilipwe baada ya kupata control number kutoka Ofisi ya Mweka Hazina wa Halmashauri ya Mtama.

ix. **MWISHO WA KUPOKEA MAOMBI NI TAREHE 21/09/2022**



**ALPHONCE O. NGONGI,
KAIMU MKURUGENZI MTENDAJI,
HALMASHAURI YA WILAYA YA MTAMA.**

**MKURUGENZI MTENDAJI (W)
HALMASHAURI YA WILAYA
MTAMA**